# AGANO LA MAOMBI
## Kwa Watoto



Mungu wa ulimwengu, Muumba wetu anasikia na kujibu maombi.Ajabu gani hiyo? Yesu alisema, ‘Kila nguvu ya mbingu na ulimwengu nimepewa’. Ikiwa Yesu ana nguvu zote, je fikiria chenye kinaweza kufanyika unapoomba…

# Neema

**Mpendwa Baba wa mbinguni,
Asante kwa kunipenda na
kunifanya mmoja wa
watoto wako.**




Yesu anataka kila mtu afahamu jinsi Mungu anavyowapenda ndipo akatoa hadithi ya mchungaji na kondoo aliyepotea.Mchungaji alikuwa anawasiwasi sana kuhusu kondoo aliyepotea hadi akawaacha kondoo wote wengine kumtafuta aliyepotea ili amwekesalama.Kondoo hawana uwezo na mara nyingine huondoka na kwenda kivyao. Wanaweza kushambuliwa na kuliwa na dubu au simba.

**Kazi ya mchungaji ni kuwalinda kondoo na hilo ndilo alifanya. Alipompata kondoo aliyepotea alifurahi sana,akambeba mikononi mpaka nyumbani na kufanya karamu kubwa kusherekea.**

**Yesu anasema hivi ndivyo itakuwa msichana au mvulana akimkubali Yesu kama mwokozi wake-wanatoka kupotea, wanapatikana. Hiyo inaleta furaha na kusherehekea mbinguni.**

**AYA YA KUMBUKUMBU**

**Tazameni jinsi Baba alivyotupenda mno, hata tukaitwa watoto wa Mungu! –1Yohana 3:1**

***Yesu anakushangilia kwa furaha,
Anakutuliza na mapenzi yake.
Anakufurahia kwa kuimba.***

# Upendo

## Nisaide nikupende na kukutii

Abrahamu alimtii Mungu,Akaondoka na mke wake,na vitu vyao vyote na kuhamia mbali kwa nyumba yao mpya.Utii wa Abrahamu ulikuwa tu mwanzo wa maisha yake kukua kwa utii,upendo na imani.




**Abrahamu alimpenda Mungu.Aliishi kitambo sana.Alipozeeka, Mungu alimwambia,'ondoka nchi yako,wacha jamii na ndungu zako naenda kwenye nchi ntakayokuonyesha.Nitakubariki na kufanya kizazi chako taifa kuu.utakuwa mashuhuri na baraka kwa watu .Kila mtu duniani atabarakiwa kwa sababu yako."**

**Mungu anataka tumtii.Tunapomtii Mungu tunamuonyesha tunampenda**

**AYA YA KUMBUKUMBU**

Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote na kwa akili zako zote. Hii ndio amri kuu, tena ni ya kwanza. –Mathayo 22:37-38

***Kumtii na kumfwata Yesu pamoja ni safari ya kusisimua!***

# Huruma

**Nisaidie kupenda wenzangu kama unavyonipenda.**

Mtu alikuwa akisafiri barabarani aliposhambuliwa na gengi la wanaume wabaya, waliompiga, kumwibia kila kitu na kumwaacha akiifa barabarani. Watu wakampita. Hawakumuonyesha huruma. Kisha Msamaria (mtu aliyedharauliwa na watu)akainama na kumtunza kwa kumsafisha vidonda na kumvika bendeji kisha kumpeleka eneo salama kupona na kulipia utunzi wake.




**Yesu alimalizia hadithi kwa kusema, “nataka mkafanyie wanaoumia kitendo kama hicho.”**

**AYA YA KUMBUKUMBU**

Amri yangu ni hii, pendaneni kama nilivyowapenda. –Yohana 15:12

***Nataka mpende kwa vitendo sio maneno tu.***

# Kutubu

**Najuta dhambi zangu.
Nisafishe nitakase.**

Kulikuwa na mfalme aliyewaiita watumishi wake wote aliye wadai. Mmoja kati yao alimdai pesa nyingi ambazo hangeweza kulipa. Mfalme akamwambia, “nitakuuza na jamii yako kama watumwa niweze kupata pesa ninakudai!” Mwanaume huyo akaanza kulia. Mfalme akaona huruma na kumwambia, “Nakuondolea deni lako, uko huru!”

Mwanaume huyo alipoachiliwa akaenda kumtafuta mfanyakazi mwenzake aliyekuwa na deni lake na kumtishia kumweka gerezani kama asipo mlipa. Mfanyakazi huyo akaamwomba huruma ila hakumuonyesha huruma na kumtupa gerezani.

Petero aliimuliza Yesu, “tusamehe mtu anatukosea mara ngapi.mara 7?” Yesu akasema “sabini mara saba” na akaanza kuwapa hadithi nyingine.




Mfalme aliposkia alikasirika na kusema kwa nguvu “Wewe mfanyakazi mwovu! Nilikusamehea deni kubwa, mbona hukumuonyesha huruma mfanyakazi mwenzako?” Na mfalme akamtupa gerezani.

**AYA YA KUMBUKUMBU**

Nioshe kabisa kutoka hatia yangu na unitakase dhambi zangu. –Zaburi 51:2

***Nataka kusemehea wenzangu kwa sababu Yesu ananisamehea.***

# Kuabudu

**Nitakusifu na moyo wangu wote!**

Yesu alipozaliwa kila mtu alifurahi! Malaika walishuka na kusema "Msifuni Mungu mbinguni! Amani duniani kwa wote wanaompendeza Mungu." Wachungaji walimtembela na kumuabudu mtoto Yesu.




Miaka mingi iliyopita zaidi ya 2000, msichana aliyeitwa Maria alitembelewa na malaika aitwae Gabriel. Alikuwa na ujumbe maalum. "Usiogope Maria, umepata upendeleo wa Mungu. Utamzaa mvulana na kumuita Yesu. Atakuwa mkuu na kuuitwa mwana wa aliyemkuu Zaidi."

Kama Maria,Yosefu ,wachungaji na wanaume wa busara walimheshimu na kumwabudu Yesu, hata sisi tunapaswa kumheshimu na kumwabudu.

**AYA YA KUMBUKUMBU**

Nitakusifu eh Bwana kwa moyo wangu wote. Nitayasimulia matendo yako yote ya ajabu. –Zaburi 9:1

***Nataka kukusifu kila siku!***

# Kujitolea

**Yesu nataka kukufuata kama Mwokozi wangu. Nibadilishe utakavyo.**

Ghafla Petero alipokumbuka maneno ya Yesu alikimbia na kulia. Alijihisi vibaya. Yesu hakumwacha Petero. Alikula kiamsha kinywa na Petero baada ya ufufuko wake na kumsamehea.Yesu alitaka Petero kuwa mfuasi wake na kupata wafuasi wengi Zaidi. Ingawaje Petero hakuwa bora kamili. Yesu alijua Petero alitaka sana kumfuata kama Bwana.




Yesu alimwambia Petero kabla jogoo liwike atamkana mara tatu.Barazani ambapo Yesu alipokuwa akihojiwa kabla ya kusulibiwa. Petero alifanya hivyo. Watu walipoanza kumtambua Petero,akawa na uoga na kila alipoulizwa alikana. Kisha jogoo likawika.

**AYA YA KUMBUKUMBU**

**Ye yote anayetaka kunifuata ni lazima ajikane nafsi yake, achukue msalaba wake kila siku, anifuate. –Luka 9:23**

**Petero hakumkana Yesu tena.**

***Yesu,nataka kuwa mwaminifu kwako kila wakati.***

# Kutegemea

**Nijaze na Roho Mtakatifu. Nataka kujua mipango yako kwangu.**

Yesu alituma Roho yake kusaidia kanisa kuanzisha  utume wake. Haikuwa siku nyingi baada ya hapo siku spesheli iitwayo Pentekosti. upepo mkali ulivuma, na kila mtu kujazwa na Roho Mtakatifu.




**AYA YA KUMBUKUMBU**

**Bali mjazwe Roho. –Waefeso 5:18b**

**Roho ya Yesu ipo nasi kila wakati kama mfariji ,mwalimu na muongozi wetu.**

***Nifanye zaidi kama wewe Yesu, kwa kunijaza na Roho Mtakatifu.***

# Ushawishi

**Nifanye mjumbe wako wa neema, ukweli na haki.**




Wafuasi walimuuliza Yesu, "Ni nani mkuu zaidi kwenye ufalme wa mbingu?" Yesu alijua wanachofikiria,akaita mtoto. Akawatazama wafuasi wake machoni na kusema kitu cha ajabu sana. "Yeyote anayejinyenyekeza kama mtoto huyu ndiye mkuu zaidi kwenye ufalme wa mbingu."

**AYA YA KUMBUKUMBU**

Tumeuona utukufu wake, utukufu wa Mwanae pekee, aliyetoka kwa Baba aliyejaa neema na ukweli. –Yohana 1:14

Yesu alikuwa na moyo wa haki. Alisema itakuwa tishio kwa yeyote atakaye waumiza watoto.Alikuwa akisaidia kila wakati wanyonge,watoto,wagonjwa na maskini

Yesu alisema kitu cha ajabu Zaidi, "Yeyote amkaribishae mtoto mdogo hivi kwa jina langu, ananikaribisha" Unajua alisema ukweli tupu.

***Nitajaribu kusema ukweli wakati wote.***

# Ufuasi

**Nitumie kwa utukufu wako niweze kualika wengine wakufuate**

Siku mmoja Saulo (kabla jina kubadilishwa kuwa Paulo) alikuwa akitembea barabarani. Ghafla akaona mwanga mkubwa utokao mbinguni uliomfanya akaanguka chini. Ukamfanya kipofu. Kisha Saulo akasikia sauti, “Saulo, mbona wanitesa?” Saulo akalia, “Wewe ni nani Bwana?” “Mimi ni Yesu ambaye unamtesa” Paulo aliogopa na kutetemeka. Kwa siku tatu hakuona.




Mungu alimponya Saulo na akaanza kuhubiri na kufundisha kuhusu Yesu kila alipoenda. Jina la Saulo lilibadilishwa baadae kuwa Paulo. Alibadilisha dunia juu chini kwa sababu ya Yesu,akimpa Mungu utukufu na kuwafundisha wengine pia kufanya hivyo.

**AYA YA KUMBUKUMBU**

Kwa hiyo nendeni mkawafanye watu wa mataifa yote kuwa wanafunzi wangu: mkiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. –Mathayo 28:19

***Ntamwalika nani kumfuata Yesu?***

# Mamlaka

## Katika jina la Yesu naomba.

"Yesu Mkuu, nihurumie!" Bartiamayo alilia.

Watu waliomzunguka Bartimayo walikua wakatili. "Jamani nyamaza!" Walimkalipia. Lakini Bartamayo akaendelea kulia.Yesu akamsikia na akasema. "Mleteni kwangu." Bartimayo akatupa koti lake na kumkibilia Yesu. "Unataka nini" Yesu alimuuliza, Bartimayo akamjibu, "Nataka kuona!"




**AYA YA KUMBUKUMBU**

**Kwa sababu hiyo Mungu alimuinua juu kabisa na akampa jina ambalo ni kuu kuliko majina yote. –Wafilipi 2:9**

***Yesu alimjibu Bartimayo alivyomlilia, hata wewe Yesu atakujibu pia.***

# Hatua za Kuchukua

1. KAAGUA AGANO LA MAOMBI
2. OMBA KWA SIKU ARUBAINI SALA LA AGANO LA MAOMBI
3. JIFUNZE KUKARIRI MISTARI YA MAOMBI YA BIBILIA
4. CHAGUA KWELI AU UONGO KISHA FAFANUA MAJIBU

| | |
|---|---|
| Neema za Mungu zimenifanya mwanae mpendwa. | UKWELI UONGO |
| Baraka hufwata na kutii. | UKWELI UONGO |
| Tunapaswa kupenda tu watupendao. | UKWELI UONGO |
| Yesu anataka tuwasamehe wengine nakutoweka kisasi. | UKWELI UONGO |
| Tunapaswa kumsifu Mungu wakati tu tunafuraha. | UKWELI UONGO |
| Tunapojitahidi kumfwata Yesu, anatufanya zaidi kama yeye. | UKWELI UONGO |
| Roho mtakatifu ndiye muongozi wetu. | UKWELI UONGO |
| Yesu hakuwa na wakati na watoto. | UKWELI UONGO |
| Mungu anatumia watu wazima peke yake kuambia wengine kuhusu Yesu. | UKWELI UONGO |
| Nguvu zote duniani na mbinguni ni za Mungu. | UKWELI UONGO |
| Maombi yana nguvu kwa sababu kuna nguvu katika jina la Yesu. | UKWELI UONGO |
| Mungu ananiskia nikiomba. | UKWELI UONGO |



# Jinsi ya kuomba AGANO LA MAOMBI Kwa Watoto

**HATUA LA 1** Omba maombi hayo peke yako kwa siku kumi

**HATUA LA 2** Unapoomba, muombe Yesu akuonyeshe ni nani utakaye mkaribisha kwa agano la maombi

**HATUA LA 3** Mwalike huyo mtu akuombee hiyo sala kwa siku arubaini nawe pia utamuombea kwa siku arubaini. Inaweza kuwa rafiki yako, mama, baba, kaka, dada, babu au nyanya, mwalimu au kasisi.

**HATUA LA 4** Shirikiana na mwenzako wa maombi jinsi Mungu anavyojibu maombi yako. Unaweza kuandika au hata kuchora picha.

**HATUA LA 5** Jifunze kukariri mistari ya bibilia iliyotengwa.

**HATUA LA 6** Eneza injili njema kuhusu Yesu na wenzako

**HATUA LA 7** Rudia maagizo haya na washirika wapya wa maombi ili muweze kumfuata Yesu pamoja.

**Jina langu ni:** ______________________

Leo nilianza kuomba Agano la Maombi la Watoto.

**Tarehe ya leo ni:** ______________

**Washirika wangu wa maombi ni**

______________ Jina ________ Tarehe

______________ Jina ________ Tarehe

______________ Jina ________ Tarehe

# AGANO LA MAOMBI
## *Kwa Watoto*

**NEEMA** Baba Mwenyezi Mungu, nakushukuru kwa kunipenda na kunifanya mmoja ya watoto wako.

**UPENDO** Nisaidie nikupende na nikutii.

**HURUMA** Nisaidie nipende wenzangu unavyonipenda.

**KUTUBU** Natubu dhambi zangu. Nitakase niwe msafi.

**KUSIFU** Nitakutukuza na moyo wangu wote!

**KUJITOLEA** Yesu nataka kukufuata. Nibadilishe vyovyote utakavyo.

**KUTEGEMEA** Nijaze na Roho Mtakatifu, nataka kujua mipango yako kwangu

**USHAWISHI** Nifanye mtumishi wako wa neema, ukweli na haki.

**UFUASI** Nitumie kwa utukufu wako niweze kualika wengine wakufuate

**MAMLAKA** Katika jina la Yesu naomba. Amina.

Hakimiliki cha ©2016 cha Candy Marballi. Haki zote zimehifadhiwa.
Vielezo na Luke Flowers. Agano la Maombi la Watoto kimechukulia kutoka Nguvu za Agano la Maombi kwa Watoto, cha Candy Marballi na Stephen Eyre

theprayercovenant.org/children

The PRAYER COVENANT For Children! | 4/14 movement | FIND US ON YouVersion